*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1) 58-79*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.4

# Utata wa Maudhui ya Kisarufi katika Vitabu vya Kiada vya *Kiswahili Kidato cha Kwanza* na *cha Tatu* Nchini Tanzania

*Alcheraus R. Mushumbwa*[1]

## Ikisiri

Vitabu vya kiada ni nyenzo muhimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili nchini Tanzania. Hutumika kama mwongozo wa ufundishaji wa mada zilizoteuliwa kwa kiwango husika cha elimu. Kutokana na umuhimu huo, vitabu hivyo huandikwa vizuri na kwa mpangilio mzuri wenye mantiki na unaoeleweka. Inapotokea kitabu cha kiada kimekuwa na changamoto za maudhui, kuna uwezekano wa maarifa yaliyokusudiwa kutowafikia walengwa kama inavyotakiwa. Hivyo basi, malengo ya makala hii ni kuchambua utata wa kimaudhui unaojitokeza kwenye vipengele vya mada za sarufi katika vitabu vya kiada vya Kiswahili (kidato I na III) na kupendekeza utatuzi wake kwa ajili ya maboresho zaidi. Data za makala hii zimepatikana kwa mbinu ya usomaji makini wa vitabu teule vilivyoandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwapo kwa utata kwenye baadhi ya vipengele vya sarufi katika vitabu hivyo. Baadhi ya utata uliobainika unahusu fasili za dhana, mifano iliyotolewa na ufafanuzi wa kushadidia hoja zilizomo vitabuni. Makala inapendekeza kuwa vitabu husika vinapaswa kupitiwa tena ili kurekebisha maudhui yanayoibua utata uliobainishwa.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inachambua utata wa maudhui unaojitokeza katika vitabu vya kiada vya Kiswahili vinavyotumika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari Tanzania. Kitabu cha kiada, kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, ni kitabu kinachoelekeza juu ya somo fulani na hutumiwa katika shule au vyuo (Radić-Bojanić na Topalov, 2016). Huu ni mwongozo unaomwelekeza mwalimu na mwanafunzi katika malengo ya somo (Nnamdi-Eruchalu, 2021). Kwa mujibu wa Radić-Bojanić na Topalov (weshatajwa), wakiwarejelea Cortazzi na Jin (1999), kitabu cha kiada kinafananishwa na mwalimu, ramani, nyenzo, mkufunzi na mamlaka. Kama mwalimu, kitabu cha kiada huwapa wanafunzi taarifa muhimu

[1] Mwalimu na Mtafiti, Shule ya Sekondari Mwang'halanga, Tanzania. Baruapepe: alche.rwega@yahoo.com

kuhusu sarufi na msamiati pamoja na utamaduni wa nchi husika. Kama ramani, kitabu cha kiada kinaonesha mwongozo wa vipengele vya kiisimu na kitamaduni kama ambavyo programu imepangwa na kinawaongoza walimu na wanafunzi kufuata hatua zilizochukuliwa katika masomo yaliyopita. Pia, kitabu cha kiada hutazamwa kama nyenzo kwa kuwa husheheni nyenzo na shughuli ambazo mwalimu anaweza kuchagua miongoni mwa zilizopendekezwa na mamlaka. Kinaweza pia kuwa kama mkufunzi kwa walimu wapya wanaohitaji maelekezo muhimu, usaidizi na mwongozo. Kama mamlaka, kitabu cha kiada hutazamwa kama chanzo halali, cha kuaminika na kilichoandikwa na wataalamu kikaidhinishwa na wachapishaji au wizara husika ya elimu. Kwa muktadha wa makala hii, kitabu cha kiada ni kitabu kilichoandaliwa (kutungwa, kuandikwa, kuchapishwa, kuidhinishwa na kusambazwa) au kupendekezwa na taasisi inayosimamia elimu ili kitumike kama mwongozo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kiwango fulani cha elimu.

Haulle na Kabelege (2021) wanaeleza kuwa kitabu cha kiada huandikwa kwa kufuata silabasi ya somo husika. Pia, wanafafanua kuwa kitabu hicho huonesha mambo yanayopaswa kufundishwa katika somo husika. Kimaudhui, kitabu cha kiada kinapaswa kuwa na mada zote za somo, maelezo yaliyo sahihi, kisiwe na makosa ya kimantiki na kiepuke kuwa na misingi hasi ya kijamii (Haulle na Kabelege, 2021:16). Kwa maana hiyo, kitabu cha kiada kinapaswa kuandikwa kwa usahihi bila makosa, utata au mkanganyiko. Kuwapo kwa utata katika vitabu vya kiada kunaweza kusababisha maudhui yanayotolewa kuzalisha maarifa kengeushi. Hivyo, makala hii inajadili utata unaopatikana katika maudhui ya mada za sarufi zilizomo kwenye vitabu vya kiada vya Kiswahili vinavyotumika katika shule za sekondari nchini Tanzania ili kuona namna utata huo ulivyo na kupendekeza utatuzi wake.

## 2.0 Mkabala wa Uchambuzi na Methodolojia ya Utafiti

Utafiti wa makala hii umeongozwa na Mkabala wa Uchanganuzi wa Maudhui (Krippendorff, 2004). Kulingana na wataalamu wa uchanganuzi wa maudhui, mkabala huu hutumika kama mwongozo na methodolojia ya utafiti wa data za kitaamuli (taz. GAO-PEMD, 1996; Krippendorff, 2004; White na Marsh, 2006). Kwanza, mkabala huu huchukuliwa kama mwongozo kwa sababu humwongoza mtafiti kulitazama jambo analotafiti na kufikia hitimisho kwa kuongozwa na sifa zake. Kulingana na waitifaki wa mtazamo huu, uchanganuzi wa kimaudhui hujumuisha usomaji makini na wa kina wa maandishi, picha au jambo lolote la kiishara ambapo maudhui huibuliwa na mtafiti kwenye mchakato wa kuchambua matini inayohusu muktadha maalumu (Kripperndorff, 2004: 3, 19). Ujumbe unaotokana na matini husika kama data ya utafiti, huibuliwa na mchambuzi kwa kuifahamu matini yake, kubuni uchanganuzi, kupanga misimbo ya kufafanua vipengele vya matini hiyo, hatimaye kufasii matokeo kulingana na uelewa wake kwa kuzingatia muktadha wa matini chunguzwa. Kama mwongozo ya makala hii,

uchanganuzi wa maudhui umemsaidia mtafiti kusoma vitabu teule vya kiada huku akichambua maudhui ya mada za sarufi na kubainisha maeneo yenye utata.

Aidha, uchanganuzi wa maudhui umetumika kama methodolojia ya uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ya makala hii. GAO-PEMD (1996) wanasisitiza kwamba mkabala huu ni mbinu ya utafiti inayotumika kwa utaratibu maalumu, kuchanganua taarifa ya matini kwa njia sanifu ambayo humruhusu mchambuzi kutoa hitimisho juu ya taarifa hiyo. Mchanganuzi hubainisha dhima/mawazo, masuala au mada ambazo anazihitaji kwa ajili ya utafiti wake. Katika makala hii, hatua za uchanganuzi wa maudhui zinazopendekezwa na Krippendorff (2004: 29-30)na White na Marsh (2006:38) zimezingatiwa kama ifuatavyo:

Hatua ya kwanza ni kupata mkusanyiko wa matini (data ya uchanganuzi). Matini za makala hii ni vitabu vya kiada vya Kiswahili vya shule za sekondari Tanzania (kidato cha I na III). Hatua ya pili ni kubainisha tatizo/swali la utafiti linaloongoza uchambuzi wa matini na data inayopatikana kutoka kwenye matini inayochambuliwa. Makala hii imechambua maudhui ya sarufi yenye utata katika vitabu vya kiada vya Kiswahili (kidato I na III). Hatua ya tatu, ni uteuzi wa sampuli (usampulishaji). Vitabu vya kiada vya Kiswahili (kidato I na III) vimeteuliwa kwa mbinu ya usampulishaji lengwa. Hatua ya nne ni usimbaji au kutafsiri data ya matini kulingana na tafsiri inayojibu maswali yanayoongoza utafiti. Hatua ya mwisho, ni kutoa mahitimisho ambayo yanakusudia kujibu swali la utafiti. Kwa kila utata uliobainishwa kwenye vitabu teule, mtafiti amehitimisha kwa kujenga hoja zinazotoa utatuzi wa utata huo.

Aidha, mbinu ya usomaji makini imetumika kukusanya data kutoka kwenye vitabu teule.Vitabu hivyo ni *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Kwanza* (2021). Kinarejelewa hapa kwa ufupisho wa KKK2021 kuwakilisha *Kiswahili Kidato cha Kwanza 2021*. Kingine ni *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tatu* (2021). Kinarejelewa hapa kwa ufupisho wa KKT2021 kuwakilisha *Kiswahili Kidato cha Tatu 2021*. Vitabu hivi vimeandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Hivyo, vimeteuliwa kuwa sampuli kwa sababu vina maelezo mengi yenye utata vikilinganishwa na vingine, kiasi kwamba, vinahitaji uchambuzi maalumu. KKK2021 na KKT2021 vimeteuliwa kwa kusoma vitabu vinne vya kiada (kidato I–IV) vilivyotungwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Baada ya kusoma vitabu hivyo, mtafiti aliteua vile vilivyokuwa na maelezo mengi yenye utata na kuvitumia kama sampuli ya utafiti huu. Kwa kuongozwa na mbinu za uchanganuzi wa maudhui zilizotajwa hapo juu, mtafiti anajenga mahitimisho kutokana na ufafanuzi wa baadhi ya vipengele vya sarufi katika vitabu teule akionesha utata unaojitokeza katika ufafanuzi huo. Data zimechanganuliwa na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyoambatana na mifano bayana ya jambo linalochunguzwa na mtafiti.

### 3.0 Utata wa Maudhui ya Kisarufi katika KKK2021 na KKT2021

Uchunguzi wa makala hii umebaini kuwapo kwa baadhi ya maelezo yenye kuibua utata katika vipengele vya silabi, sauti za Kiswahili, aina za maneno, ngeli za nomino, kirai, kishazi, kiarifu na sentensi. Utata huu unaonekana kwenye fasili za baadhi ya dhana, mifano iliyotolewa, au ufafanuzi wa kushadidia hoja zilizomo vitabuni humo. Uchambuzi wa utata huo unafanyika kwenye vipengele vifuatavyo.

### 3.1 Utata wa Maudhui ya Kisarufi katika KKK2021

Katika kitabu hiki, kuna maelezo, mifano na hoja ambazo zinaibua utata au mkanganyiko kwa wasomaji kama inavyofafanuliwa.

#### 3.1.1 Dhana ya Silabi

Dhana ya silabi imefafanuliwa kwa namna ambayo inaacha maswali yenye kuibua utata au mkanganyiko kwa msomaji. Maana, mifano na miundo ya silabi iliyoelezwa kwenye KKK2021 ina uvuliuvuli ambao unapaswa kuangaliwa upya. Kwa kuanza na maana ya silabi, katika kitabu hicho imefafanuliwa kuwa "ni sehemu ya neno *inayoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake*[2] na hutamkwa kwa pamoja na mara moja kama fungu moja la sauti" (TET, 2021:13). Katika fasili hii, waandishi wanajumuisha muundo wa silabi kama sehemu muhimu ya kufasili dhana hiyo. Utata unaibuka ambapo miundo ya silabi iliyotajwa ni miwili tu wakati kuna miundo zaidi ya hiyo. Hakukuwa na haja ya fasili ya silabi kuhusisha muundowa silabi. Kama kuna umuhimu wa kufanya hivyo, fasili ilipaswa kutaja miundo yote na siyo miwili tu. Hata hivyo, kufanya hivyo, kunahitaji kuorodhesha miundo yote kwenye fasili, jambo ambalo ni gumu.

Pili, utata mwingine uko kwenye kutaja baadhi ya miundo ya silabi na kuacha mingine bila maelezo ya kufanya hivyo. Kwa mujibu wa kitabu hicho, miundo ifuatayo imeorodheshwa:

1. Mifano ya miundo ya silabi kwa mujibu wa KKK2021 ni kama:
   (i) Irabu pekee: Mfano, silabi **a** na **u** katika neno *ua;*
   (ii) Konsonanti moja na irabu moja: Mfano, silabi **la** na **la** katika neno *lala*;
   (iii) Konsonanti mbili au zaidi na irabu moja: Mfano, silabi **mba** katika neno *shamba*;
   (iv) Konsonanti moja na kiyeyusho kimoja na irabu moja: Mfano, silabi **pya** katika neno *jipya*;
   (v) Konsonanti mbili, kiyeyusho kimoja na irabu moja: Mfano, silabi **mbwa** katika neno *pambwa*.

   **Chanzo**: TET (2021:13)

[2] Hati mlazo kwenye mifano au data kutoka kwenye vitabu vinavyochambuliwa ni msisitizo wa mwandishi wa makala hii. Umetumika pia kuweka bayana jambo linalolengwa.

Kama ambavyo Mfano Na. 1(i)–(v) unaonesha, ni wazi kuwa kuna baadhi ya miundo ya silabi haikutajawa. Mathalani, muundo wa konsonanti pekee (ambao huundwa na nazali) kama ***m**-toto*, ***n**-ta* haukutajwa. Pia, kuna baadhi ya miundo ya silabi ambayo maneno yake yamekopwa kutoka lugha za kigeni (Massamba na wenzake, 2004) haikuorodheshwa kama sehemu ya miundo ya silabi za Kiswahili. Kwa mfano, maneno ya mkopo kama *labda*, *sekta*, *daftari*, *faksi* n.k. yanaundwa na silabi zenye miundo tofauti na iliyotajwa kwenye KKK2021. Kuna muundo wa *konsonanti konsonanti na irabu (KKI)* ambao unatofautiana kidogo na ule wa silabi za Kiswahili za maneno ya asili ya Kibantu. Katika muundo huu, hakuna nazali wala kiyeyusho kama kwenye neno *la-**bda***, *se-**kta***, *da-**fta**-ri*, *fa-**ksi*** [3] (Massamba na wenzake, 2004; Ligembe, 2017). Miundo ya namna hii isipotajwa, humpa mwanafunzi wakati mgumu wa kubainisha silabi katika maneno ya mkopo kama hayo.

Kulingana na utata uliojitokeza kwenye dhana ya silabi, inapendekezwa kuwa utata huo unaweza kuondolewa kama fasili ya silabi haitahusisha miundo yake. Kwa mantiki hiyo, silabi ingefasiliwa kuwa ni sehemu ya neno ambayo hutamkwa kwa pamoja na mara moja kama fungu moja la sauti. Pia, waandishi wasingeweka ukomo wa miundo ya silabi za Kiswahili kwa kusema kuwa "muundo wa silabi za Kiswahili unajibainisha katika miundo ifuatayo …" (KKK2021, uk.13).Wangeweza kuandika kuwa silabi za Kiswahili hujibainisha katika miundo mbalimbali na miongoni mwao ni ile iliyobainishwa kwenye kitabu hicho. Hata hivyo, kwa kuwa ni kitabu cha kiada, kinapaswa kubainisha miundo yote inayojidhihirisha katika silabi za lugha ya Kiswahili.

#### 3.1.2Aina za Sauti za Kiswahili

Waandishi wa kitabu cha KKK2021 wanaeleza kuwa sauti zimegawanyika katika aina mbili ambazo ni irabu na konsonanti (uk.15). Uainishaji huu unakinzana na maelezo yaliyotolewa katika ukurasa wa 13 wa kitabu hicho yanayobainisha makundi ya sauti zilizounda miundo ya silabi. Mfano wa Na. 2 unaonesha ufafanuzi huo.

2. Irabu za Kiswahili ni **a, e, i, o** na **u**. Konsonanti za Kiswahili ni **b, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, l, m, n, ng', ny, p, r, s, sh, t, th, v** na **z**. Viyeyusho katika lugha ya Kiswahili ni **w** na **y** (TET, 2021: 13).

---

[3]Upo mtazamo unaodai kwamba silabi zilizobainishwa hapo juu kama muundo wa KKI kutoka kwenye maneno ya mkopo ni silabi mbili na wala sio moja kama ilivyobainishwa na Massamba na wenzake (weshatajwa) na Ligembe (keshatajwa). Kwa mtazamo huo, maneno hayo yanatengwa kama *la-**b**-da*, *da-**f**-ta-ri*, *fa-**k**-si*, *se-**k**-ta*. Hata hivyo, tukumbuke kuwa silabi hubainishwa kutokana na sauti inavyosikika katika utamkaji kama fungu moja na sio inavyoonekana. Utamkaji wa maneno hayo unatuonesha kuwa sauti zilizokolezwa wino hazitamkwi pekee kama fungu moja bali humezwa na sauti zinazofuata. Ikiwa zitatengwa kama silabi basi itabidi iwe "la-**bu**-da, da-**fu**-ta-ri, fa-**ki**-si, se-**ki**-ta", jambo ambalo sio sahihi katika utamkaji wa Kiswahili sanifu. Hivyo, tunakubaliana na mtazamo wa utengaji wa Masssamba na wenzake na Ligembe wa kuzitenga silabi hizo kama *la-**bda***, *da-**fta**-ri*, *fa-**ksi***, na *se-**kta***.

Tukiangalia uainishaji wa sauti za Kiswahili katika ukurasa wa 15 na maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa katika ukurasa 13 kuhusu sauti zinazounda silabi, ni wazi kuwa yanamchanganya msomaji kwa sababu katika ukurasa wa 13, sauti za Kiswahili zinaainishwa katika makundi matatu ilhali katika ukurasa wa 15 sauti hizohizo zinaainishwa katika makundi mawili bila kuwapo kwa maelezo ya msingi ya kufanya hivyo. Hali hii inazua utata kwa walimu na wanafunzi. Kwa mfano, wanafunzi waliosoma kitabu hicho wakiulizwa wataje makundi ya sauti za Kiswahili, kuna ambao watataja konsonanti na irabu na kuna ambao watataja konsonanti, irabu na viyeyusho. Majibu haya yanadokeza umahiri tofauti kwa wanafunzi walewale wa kiwango kimoja. Je, mwalimu afuate mwelekeo upi?

Ili kuondoa mkanganyiko huo, waandishi wa KKK2021 walipaswa kuwa na msimamo mmoja ama kwa kutaja makundi mawili ya sauti za Kiswahili (konsonanti na irabu) au makundi matatu (konsonanti, irabu na viyeyusho). Ikumbukwe kuwa uainishaji wa sauti za Kiswahili katika kitabu hicho umezingatia sifa za matamshi ya sauti hizo–jinsi sauti za Kiswahili zinavyotamkwa. Kwa msingi huo, ingelikuwa vyema kuchagua kundi mojawapo. Hata hivyo, uainishaji wa konsonanti, irabu na viyeyusho ungefaa zaidi kwa sababu, viyeyusho haviko katika kundi la konsonanti moja kwa moja au irabu moja kwa moja bali viko katikati. Hii inamaanisha kuwa viyeyusho hubeba baadhi ya sifa za konsonanti na zile za irabu na kuunda kundi lake (Massamba na wenzake, 2004: 28; Matinde, 2012:73; Ligembe, 2017:25).

### 3.1.3 Aina za Maneno

Baadhi ya maelezo yanayohusu aina za maneno katika KKK2021 yanazua maswali yenye utata na mkanganyiko. Utata huo unadhihirika katika vipengele vya viwakilishi na vivumishi, nomino, vitenzi, viunganishi na vihusishi. Ufuatao ni ufafanuzi wa utata huo.

#### 3.1.3.1 Viwakilishi na Vivumishi

Utata wa kwanza unahusu uainishaji wa viwakilishi kwa kutaja aina sita tu za viwakilishi. Kwa mujibu wa KKK2021, viwakilishi vimegawanyika katika makundi sita ambayo ni viwakilishi vya nafsi, idadi, vimilikishi, viulizi, vioneshi na vya pekee (TET, 2021: 24). Maelezo haya yanazua utata na mkanganyiko kwa walimu na wanafunzi ambao wamesoma vitabu vingine ambavyo vimeainisha aina za viwakilishi zaidi ya sita. Kwa mfano, kuna viwakilishi vya amba/rejeshi na viwakilishi vya sifa ambavyo havikutajwa katika kitabu hicho. Mathalani, katika sentensi zifuatazo, viwakilishi virejeshi na sifa vinadhihirika.

3. (a) ***Ambaye*** alikuja jana ametoroka.
   (b) Hakufurahia ***ambacho*** ulisema.
   (c) ***Wabaya watachomwa*** siku ya kiama.
   (d) ***Kizuri*** chajiuza.
   **Chanzo**: Matinde (2012: 138).

Katika Mfano Na. 3(a)-(b), maneno yaliyokolezwa wino na kuandikwa kwa mlazo ni viwakilishi virejeshi/amba na maneno yaliyokolezwa wino na kuandikwa kwa mlazo katika Mfano Na. 3(c)-(d) ni viwakilishi vya sifa. Aidha, makala hii inatambua kuwa kuna kutofautiana kwa waandishi wa vitabu vya sarufi ya Kiswahili katika uainishaji wa kategoria ya kiwakilishi. Kuna wanaotaja aina tisa (Bukagile, 2007; Matinde, 2012), sita (Habwe na Karanja, 2004; Ndumiwe, 2021) na tano (Kihore na Wenzake, 2003; Philipo, 2018). Waandishi wa KKK2021 wanaingia katika kumbo la walioainisha aina sita. Kwa kutambua utofauti wa aina za viwakilishi miongoni mwa waandishi, waandishi wa KKK2021 walipaswa kutoa ufafanuzi kwa nini wameamua kuainisha aina sita tu na si zingine. Ufafanuzi huo ungeondoa utata.

Utata mwingine unajitokeza katika ufafanuzi wa uamilifu wa kiwakilishi na kivumishi. Ufafanuzi huo uko kama ifuatavyo:

> Kwa kuwa kiwakilishi hutumika badala ya nomino, ni dhahiri kuwa *nomino na kiwakilishi haviwezi kutokea mahali pamoja* katika sentensi. *Ikitokea hivyo, kiwakilishi kitabadilika hadhi na kuwa kivumishi*. Tazama mifano ifuatayo:
>
> ***Mwenyewe*** hakujali.
>
> Dereva ***mwenyewe*** hakujali.
>
> Katika sentensi ya 1 neno ***mwenyewe*** ni kiwakilishi wakati katika sentensi ya 2 neno ***mwenyewe*** ni kivumishi.
> **Chanzo:** KKK (2021: 24-25).

> Kwa kuwa kivumishi husifia au hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi, ni dhahiri kuwa kivumishi hutumika ikiwa kuna nomino au kiwakilishi. Ikiwa kivumishi kitabaki bila nomino au kiwakilishi, *kitapoteza sifa ya kuwa kivumishi*. Katika muktadha huo, kitabeba dhima ya kiwakilishi. Chunguza mifano ifuatayo:
>
> (a) Mtoto ***mzuri*** amekuja.
> (b) ***Mzuri*** amekuja.
>
> Katika mfano (a) neno **mzuri** ni kivumishi wakati katika sentensi (b) neno **mzuri** ni kiwakilishi.
> **Chanzo:** KKK (2021: 25-26).

Katika nukuu ya kwanza kuhusu uamilifu wa kiwakilishi, tunakubaliana na maelezo ya kwamba kiwakilishi na nomino haviwezi kutokea mahali pamoja kwenye tungo na vikatimiza majukumu yake. Hata hivyo, tunapata shaka na ukweli wa kauli inayosema kuwa "ikitokea hivyo (kiwakilishi na nomino kukaa pamoja), kiwakilishi kitabadilika hadhi na kuwa kivumishi." Kauli hiyo ina changamoto ya kimantiki kwani ni vigumu kiuamilifu, kiwakilishi kubadilika hadhi na kuwa kivumishi. Hii ni kusema kuwa, viwakilishi vyote vina maumbo huru yasiyobadilika, yanayovitambulisha kama aina ya maneno. Kauli hiyo pia

inalenga kudokeza kwamba, dhana ya kiwakilishi si ya kiuamilifu bali ni ya kiumbo, jambo ambalo linatia shaka. Kwa mujibu wa maandiko mbalimbali ya sarufi ya Kiswahili, kiwakilishi ni dhana ya kiuamilifu kama ilivyo nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kiunganishi, kihusishi n.k. na umbo la kiwakilishi huundwa na kiambishi cha upatanisho wa kisarufi na mzizi (Kihore na wenzake, 2003:150-163; Matinde, 2012:135-138). Tazama mifano katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1: Mifano ya Maumbo ya Viwakilishi**

| Mzizi | Muundo wa Kiwakilishi | Kiwakilishi |
|---|---|---|
| **(a) -zuri** | M+**zuri**/wa+**zuri** | Mzuri/wazuri |
| | Ki+**zuri**/vi+**zuri** | Kizuri/vizuri |
| | Ø+**zuri**/ma+**zuri** | Zuri/mazuri |
| | M+**zuri**/mi+**zuri** n.k | Mzuri/wazuri |
| **(b) -enyewe** | Mu+**enyewe**/u+**enyewe** | Mwenyewe/wenyewe |
| | Ki+**enyewe**/vi+**enyewe** | Chenyewe/vyenyewe |
| | Li+**enyewe**/mi+**enyewe** | Lenyewe/yenyewe |
| | u+**enyewe**/i+**enyewe** n.k | Wenyewe/yenyewe |
| **(c) -refu** | m+refu/wa+**refu** | Mrefu/warefu |
| | ki+refu/vi+**refu** | Kirefu/virefu |
| | Ø+**refu**/ma+**refu** | Refu/marefu |
| | m+**refu**/mi+**refu** n.k | Refu/mirefu |
| **(d) -baya** | m+**baya**/wa+**baya** | Mbaya/wabaya |
| | ki+**baya**/vi+**baya** | Kibaya/vibaya |
| | Ø+**baya**/ma+**baya** | Baya/mabaya |
| | m+**baya**/mi+**baya** | Mbaya/mibaya |

**Chanzo**: Uwandani (2023)

Tukichunguza mifano ya Jedwali Na.1, tunabaini kuwa umbo la kiwakilishi huundwa na vipashio funge isipokuwa viwakilishi vya nafsi. Maumbo ya viwakilishi vingine ambavyo si vya nafsi hubadilika kulingana na kipatanishi chake katika umoja na wingi. Maelezo haya yana maana kuwa mizizi ya viwakilishi hupokea viambishi awali vipatanishi ili kuunda umbo kamili (neno) lenye uamilifu wa uwakilishi katika tungo. Hivyo, kusema kuwa kiwakilishi kinapoambatana na nomino kinabadilika hadhi na kuwa kivumishi ni kuzua utata. Nomino huambatana na kivumishi pamoja na maneno mengine kwenye mpangilio wa tungo lakini sio kiwakilishi. Ingetosha kusema, kwa kuwa kiwakilishi huwakilisha nomino, basi hakuna uwezekano wa nomino na kiwalikishi kuambatana pamoja na vikafanya kazi ileile kwenye tungo moja.

Maelezo yaliyotolewa awali kuhusu kiwakilishi, hayatofautiani sana kwa upande wa kivumishi. Kwa upande mwingine, kivumishi nacho ni dhana

inayobainishwa kulingana na uamilifu wake kwenye tungo. Ni vigumu kubainisha umbo huru la kivumishi kama aina ya maneno isipokuwa umbo la kivumishi hujengwa na vipashio funge. Umbo hilo likiandamana na nomino/kiwakilishi huwa na jukumu la kuvumisha au kutoa sifa juu ya nomino/kiwakilishi husika. Kwa mantiki hiyo, mzizi funge hupokea kiambishi cha upatanisho wa kisarufi (Matinde, 2012:128-134) na kuunda umbo ambalo likiambatana na nomino/kiwakilishi huitwa kivumishi (likiwa linasifia kuhusu nomino hiyo). Kwa mfano, katika virai nomino (i) Mtoto **mzuri**, (ii) Mtu **mwenyewe** (iii) Mji **mbaya** n.k., maneno yaliyokolezwa wino kwenye miandamo hiyo ni vivumishi kwa kuwa vinafafanua juu ya nomino ambazo zimeandamana navyo.

Tunaona fika kuwa mzizi {**zuri**, **enyewe**, **baya**} iliyotumika kuunda viwakilishi katika ufafanuzi wa aya ya juu, imetumika pia kuunda vivumishi kwa kuambikwa viambishi awali vipatanishi (m, mw, m} kwenye virai (i)–(iii). Maelezo haya yanatufanya kukubali kwamba, kivumishi hakiwezi kubaki peke yake kikabadilika hadhi na kuwa kiwakilishi kwa sababu ili kiwe kivumishi ni lazima kiwe kimeambatana na nomino katika tungo. Kwa mantiki hii, hakukuwa na haja ya kusema kwamba kivumishi kinapokaa peke yake bila nomino au kiwakilishi hupoteza sifa yake na kubeba dhima ya kiwakilishi.

Aidha, katika kutaja aina za vivumishi, waandishi wa KKK2021 wanabainisha kwamba kuna kivumishi cha a-unganifu kwa kutoa mifano kama "*wa Juma*, *la heri* na *cha mama*" (uk.26). Aina hii ya kivumishi na mifano yake inazua utata kwa sababu katika kitabu hichohicho kuna kihusishi kama aina ya neno iliyobainishwa. Kwa mfano, maneno hayo yaliyojatwa kama mifano ya vivumishi vya a-unganifu yakiambatanishwa na nomino/viwalikishi ili yatimize majukumu yake yatakuwa kama ifuatavyo:

4. (a) Mkoba ***wa*** Juma
   (b) Jambo ***la*** heri
   (c) Kitenge ***cha*** mama
   **Chanzo**: Uwandani (2023)

Katika Mfano Namba 4(a)-(c), maneno yaliyokolezwa wino ni vihusishi vinavyohusisha nomino zinazounda vipashio hivyo. Hivyo, inaleta ukakasi kudai kuwa kuna kivumishi cha a-unganifu ikiwa tayari kuna kihusishi kama aina ya neno. Zaidi ni kwamba, maneno yaliyotolewa mifano kama vivumishi vya a-unganifu katika KKK2021 (uk.26) ni vikundi vya maneno na kama ni vikundi vya maneno, basi hayako tena katika kategoria ya neno bali ni kirai. Kwa maelezo haya, ni wazi kuwa dhana ya kivumishi cha a-unganifu inakosa mashiko kwa sababu kama ilivyooneshwa kwenye mifano namba 5 hapo juu, maneno yanayodaiwa kuwa vivumishi vya a-unganifu yanafanya kazi ya kihusishi. Hivyo, ni vihusishi na si vivumishi.

**3.1.3.2 Nomino**

Katika ufafanuzi wa aina za nomino, waandishi wa KKK2021 wanaeleza kwamba nomino za pekee, pamoja na mambo mengine, zinaweza kutaja vyeo vinavyoambatana na majina mahususi. Wanatoa mfano wa "*Mwenyekiti Joni* (uk.23)". Hata hivyo, maelezo haya yanakinzana na yaliyotolewa katika ukurasa wa 26 yakifafanua kuhusu kivumishi kwamba "*baadhi ya nomino hufanya kazi ya kivumishi kwa vile huzifafanua nomino zingine. Nomino hizi huitwa vivumishi vya jina: kwa mfano, Mwalimu **Hamisi** na Katibu **Kata***" (TET, 2012:26).

Pamoja na kwamba nukuu iliyotolewa hapa inakinzana na maelezo yaliyotolewa kuhusu nomino mahususi kutajwa kwa majina na vyeo vyake, pia utata unaojitokeza katika maelezo hayo ni kutofafanua kati ya **Mwalimu** na **Hamisi** au **Katibu** na **Kata**ni nomino ipi inayovumisha nyingine? Ikiwa nomino zilizokolezwa wino kwenye mifano hiyo ndizo zinazofanya uvumishaji, basi kunaibuka swali ambalo litapaswa kufafanuliwa na kupewa majibu yakinifu kwamba, neno "Hamisi" ni nomino mahususi na "mwalimu" ni cheo (nomino ya kawaida). Je, nomino mahususi inaweza kuvumisha nomino ya kawaida au nomino ya kawaida ndiyo yenye jukumu la kuvumisha nomino mahususi? Ikiwa tutakubaliana kuwa nomino mahususi ndiyo inayovumisha nomino ya kawaida, basi maelezo yaliyotolewa kuhusu nomino mahususi kuambatana na vyeo, yatakuwa yanakosa mantiki. Hivyo basi, waandishi wa KKK2021 wana haja ya kutafakari upya dhana ya "nomino kivumishi" na "nomino pekee inayoambatana na cheo" ili kutoa maelezo yasiyosigana kwa sababu nomino zaidi ya moja zinaweza kufuatana lakini sio lazima moja iwe kivumishi.

**3.1.3.3 Viunganishi na Vihusishi**

Kuna maelezo yanayoibua mkanganyiko katika kufasili kiunganishi na kihusishi pamoja na mifano yake. Kwa mujibu wa KKK2021, kiunganishi na kihusishi vinapambanuliwa kama ifuatavyo:

> Kiunganishi hutumiwa kuweka pamoja au kuunganisha pande mbili zenye hadhi sawa kisarufi. Pande hizo zinaweza kuwa neno na neno kama vile nomino na nomino au kitenzi na kitenzi au kifungu cha maneno na kifungu kingine cha maneno. Kwa hiyo, huwezi kuunganisha aina tofauti za maneno kama kitenzi na nomino. … Vihusishi vinaonesha uhusiano kati ya neno na neno au kifungu cha maneno na kifungu kingine. Tofauti na ilivyo kwa viunganishi, vihusishi huhusisha tungo zenye hadhi tofauti kisarufi… Tofauti kubwa kati ya kiunganishi na kihusishi ni hadhi ya maneno au vifungu vya maneno vinavyounganishwa na kuhusishwa. Ikiwa vina hadhi sawa kitakuwa kiunganishi na ikiwa vina hadhi tofauti kinakuwa kihusishi
>
> **Chanzo:** TET (2021: 28-29).

Maelezo hayo yanasisitiza hadhi ya vipashio vinavyounganishwa katika tungo ili kupata utofauti kati ya kategoria ya kiunganishi na kihusishi. Hata hivyo, utata

unaibuka pale kihusishi kinapohusisha maneno yenye hadhi sawa katika tungo.Tazama Mfano Na. 5 hapa chini:

5. (a) *Hali* ***ya*** *hewa* ni nzuri.
   (b) *Kitabu* ***cha*** *Kiswahili kimepotea*.
   (c) *Mtoto* ***wa*** *mwalimu amefaulu*. n.k
   **Chanzo**: Uwandani (2023)

Katika Mfano Na. 5 (a)–(c), maneno yaliyokolezwa wino yanahusisha tungo zenye hadhi sawa – zote ni nomino. Kwa uamilifu wake katika tungo hizo, maneno "**ya**, **cha** na **wa**" ni vihusishi siyo viunganishi japo yanahusisha tungo zenye hadhi sawa kisarufi. Hivyo, tunaona kuwa kigezo cha "hadhi ya tungo" zinazounganishwa hakitoshelezi kufasili na kutofautisha kategoria ya kihusishi na kiunganishi. Ingefaa uamilifu wa neno linalosadikika kuunganisha au kuhusisha maneno mengine ukazingatiwa pia.

### 3.2 Utata wa Maudhui ya Kisarufi katika KKT2021

Katika KKT2021 yamebainika baadhi ya maelezo kwenye mada za sarufi yenye kuzua utata. Baadhi ya vipengele vinavyochambuliwa sehemu zinazofuata ni ufafanuzi wa uainishaji wa ngeli, kirai, kishazi, kiarifu na sentensi.

#### 3.2.1 Uainishaji wa Ngeli

Ngeli hufafanuliwa kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi katika ngazi ya kidato cha tatu (TET, 2010). Katika kueleza kigezo hicho, waandishi wanasema "upatanisho wa kisarufi hutambulisha ngeli za nomino kwa kuangalia viambishi awali vya umoja na wingi katika nomino au viwakilishi, vivumishi na vitenzi katika sentensi. Hivyo, uainishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi huzingatia viambishi awali vya nomino au viwakilishi, vivumishi na vitenzi" (TET, 2021:5). Kwa mfano, a Jedwali Na. 2 linaonesha baadhi ya ngeli kutoka KKT2021:

**Jedwali Na. 2: Mifano ya Ngeli Kulingana na KKT 2021**

| Aina ya Ngeli | Viambishi | Mifano katika Sentensi |
|---|---|---|
| **YU/A – WA** | YU/A – umoja<br>WA – wingi | Mgeni **yu**mo ndani/mgeni **a**mekuja<br>Wageni **wa**mekuja |
| **U – I** | I – wingi<br>U – umoja | Mikutano **i**meanza<br>Mkutano **u**meanza |
| **LI – YA** | LI – umoja<br>YA – wingi | Majembe **ya**mepotea<br>Jembe **li**mepotea |
| **KI – VI** | KI – umoja | Kijiko **ki**nang'aa |

| | | |
|---|---|---|
| | VI – wingi | Vijiko **vi**nang'aa |
| **I – ZI** | ZI – wingi | Kazi hizi **zi**natosha |
| | I – umoja | Kazi hii **i**natosha |

**Chanzo**: TET (2021:7)

Kwa kuzingatia mifano ya Jedwali Na. 2 na ufafanuzi uliotolewa kuhusu uainishaji wa ngeli kwenye KKT2021, msomaji anaweza kukanganyika kwa sababu maelezo hayaakisi mifano ya ngeli iliyotolewa kwenye kitabu hicho. Kulingana na data ya Jedwali Na. 2, viambishi awali vya vitenzi vilivyokolezwa wino ndivyo vinavyozingatiwa na kuchukua jukumu la kuwakilisha ngeli husika. Utaratibu huo ndio unaotumika katika uainishaji wa ngeli kwa kigezo cha kisintaksia. Kwa hiyo, kuhusisha viambishi awali vya nomino na vivumishi katika fasili hiyo kunaibua mkanganyiko ambao haukuwa wa lazima. Ikiwa kama ambavyo maelezo ya KKT2021 yanasema, itamaanisha kuwa kila kundi la ngeli litapaswa kuwakilishwa na viambishi awali vya nomino, vivumishi na vitenzi husika. Jambo ambalo linakuwa gumu kutekelezeka kwa sababu:

(i) Maumbo ya viambishi awali vya nomino hutofautiana katika baadhi ya nomino hata zile zenye sifa zinazofanana, mathalani, ***m**tu/**wa**tu*, ***ki**pofu/**vi**pofu*, ***ki**ziwi/**vi**ziwi* n.k. Nomino hizi zina sifa ya viumbe hai lakini zinatofautiana kwenye maumbo ya umoja na wingi.
(ii) Viambishi awali vya nomino sio vyote vinavyofanana na vile vya vivumishi vinavyofafanua nomino husika, mathalani, ***m**ti **u**le/**mi**ti **i**le*, *bati **l**angu/**ma**bati **y**angu* n.k.
(iii) Si kila nomino inapokea viambishi awali vya umoja na wingi, zingine zina vile vya umoja au vya wingi tu au hazina vyote kwa pamoja, mathalani *meza/meza*, *simu/simu*, *sahani/sahani*, *hakimu/**ma**hakimu*, *kombe/**ma**kombe* n.k.

Kwa msingi huo, inakuwa vigumu kuunda jina la ngeli kwa kuzingatia viambishi awali vya umoja na wingi vinavyobebwa na nomino, vivumishi na vitenzi kwa pamoja. Aidha, vitenzi ndivyo vinavyopokea kwa kiasi kikubwa viambishi awali vinavyowakilisha nomino husika kwa msingi wa upatanisho ambapo viambishi hivyo hufanana angalau kwa nomino nyingi za kundi husika. Inashauriwa kwamba ingekuwa vyema waandishi wa KKT2021 wakasisitiza kuwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi huzitenga ngeli kwa kuangalia uhusiano wa upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kitenzi ambapo kundi la ngeli huwakilishwa na viambishi awali vipatanishi vinavyowekwa katika vitenzi. Wakisisitiza hoja hii, Kihore na wenzake (2003:98) wanasema kwamba kiambishi cha upatanisho wa kisarufi kilichochaguliwa ni kile ambacho huambikwa kwenye kitenzi.

### 3.2.2 Kirai

Miongoni mwa sifa za kirai zilizofafanuliwa katika KKT2021 nikuwa hakina muundo wa kiima na kiarifu. Sifa hii inazua utata pale inapotumia vipashio vya kidhima/kikazi kufasili kirai ambacho ni kipashio cha kimuundo. Akikosoa fasili zinazoeleza muundo wa kirai kwa kutumia dhana za kiima na kiarifu, Ndumiwe (2021:28) anasema kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo ambacho kinaundwa na neno kuu na kijalizo au neno kuu peke yake aghalabu hakina muundo wa KN na KT kwa pamoja. Makala hii inaunga mkono fasili ya Ndumiwe (keshatajwa) kwa kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo, hivyo, istilahi zinazokifasili zinapaswa kuwa za kimuundo kuliko za kidhima.

### 3.2.3 Kishazi

Kipengele hiki nacho kimezua utata katika ufafanuzi wake. Kwanza, utata unajitokeza kwenye fasili ya kishazi. Kwa mujibu wa KKT2021, kishazi ni "neno au mpangilio *wenye kitenzi kimoja* ndani yake" (uk.29). Maana hii inafunga mipaka ya kuwa na kishazi chenye vitenzi viwili au zaidi. Hii inamaanisha kuwa kishazi hakiwezi kuwa na vitenzi zaidi ya kimoja. Fasili hiyo basi, haitambui vishazi vyenye miundo ifuatayo katika sentensi kwenye Mfano Na. 6(a)-(d) hapa chini.

6. (a) Mtoto ***aliyekuwa analia*** amenyamaza.
   (b) Wale ***waliokuwa wanataka kumpiga*** walidhibitiwa na askari.
   (c) Nilivyomuona ***alitaka kukimbia***.
   (d) Barua uliyoniletea ***ilikuwa imechanika***.
   **Chanzo**: Uwandani (2023)

Kwa kutazama Mfano Na. 6(a)-(d) ni wazi kuwa vishazi vilivyobainishwa kwa wino mzito vimeundwa na vitenzi zaidi ya kimoja. Kwa hiyo, kusema kishazi ni tungo yenye kitenzi kimoja ndani yake ni kutupilia mbali uwezekano wa kishazi kuwa na vitenzi zaidi ya kimoja. Hivyo, inashauriwa fasili ya kishazi isiwekewe mipaka ya idadi ya vitenzi.

Pili, katika kutaja sifa za vishazi, imeelezwa kuwa kishazi kimojawapo katika sentensi huwa na o–rejeshi au kiambishi cha masharti (TET, 2021: 29). Sifa hii inatueleza kuwa ni lazima sentensi iundwe na vishazi viwili tofauti (kishazi tegemezi na huru) na kusahau kuwa kuna sentensi zinazoundwa na kishazi huru kimoja au zaidi hasa sentensi sahili na ambatani. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2012: 124), vishazi ambatani ni vishazi ambavyo vimeunganishwa katika sentensi kuu na viunganishi na sifa mojawapo ni ile ya kuwa huru. Kwa mfano:

7. (a) *Sijui* wala *sijali*
   (b) *Unaudhi* tena *unanichefua*
   **Chanzo:** Massamba na wenzake (2012:124).

Katika Mfano Na. 7 (a)–(b) ni wazi kuwa maneno yaliyoandikwa kwa mlazo ni vishazi huru. Vishazi hivyo havina kiambishi cha o–rejeshi wala masharti japo

vipo kwenye sentensi moja. Pia, hata katika sentensi changamani inayoundwa na kishazi huru na kishazi tegemezi, bado kuna muundo ambao utegemezi wa kishazi hauegemei kwenye kiambishi rejeshi au masharti kama sentensi "***Ingawa tumefika*** *hatukumuona*" na "***Hatakama utakuja*** *hutanikuta*." Katika sentensi hizi kuna vishazi tegemezi ambavyo havijaundwa na o–rejeshi wala kiambishi cha masharti. Kwa hiyo, kusema kuwa kishazi kimojawapo ndani ya sentensi huwa na o–rejeshi au kiambishi cha masharti ni kufunga ufikiri wa mwanafunzi na mwalimu juu ya miundo mbalimbali ya vishazi vinavyounda sentensi.

Tatu, utata mwingine unajitokeza katika miundo ya kishazi huru pale ambapo muundo uliotajwa na mfano wake havioani. Imetajwa kuwa kishazi huru huundwa na kitenzi kishirikishi na kutoa mfano wa "Kijana aliyeondoka *si* mwalimu wetu" (uk.33). Katika mfano huu, kipashio kilichobainishwa kwa hati mlazo hakikidhi ukweli wa muundo uliotajwa. Tulitegemea muundo wa sentensi hiyo uwe na kishazi huru kinachoundwa na kitenzi kishirikishi tu kinachojitosheleza kimaana ila si kama ilivyobainishwa kwenye sentensi ya mfano. Kwa jinsi sentensi ilivyo, ni wazi kuwa kishazi huru ni "kijana si mwalimu wetu." Kitenzi kishirikishi "si" katika tungo hii hakijitoshelezi kitaarifa isipokuwa kinapoambatanishwa na kijalizo "mwalimu wetu" ndipo kinapoifanya sentensi kukamilika kitaarifa. Hivyo, kwa kuzingatia muundo uliotajwa, kishazi huru kingekuwa ni ***"siye"*** katika sentensi "*Kijana aliyeondoka* ***siye"***.

### 3.2.4 Kiarifu

Ufafanuzi wa kiarifu unaibua utata pia. Kwanza, utata unadhihirika katika miundo ya kipashio hicho iliyotajwa. Miongoni mwa miundo iliyobainishwa ndani ya KKT2021 ni muundo wa kitenzi kishirikishi na mfano uliotolewa ni "Maua ni *mkulima hodari*" (uk.36). Katika mfano huu, maneno yaliyobainishwa kama kiarifu siyo kiarifu bali ni sehemu ya kiarifu. Hali kadhalika, kipashio kilichotajwa kuwa ndicho kinachounda kiarifu hakikubainishwa. Ikiwa maneno yaliyobanishwa ni kiarifu, bado jambo hilo litakuwa si sahihi kwa sababu hakuna kitenzi kinachoarifu ambacho ni kiini cha kiarifu. Hivyo, mfano huo unaleta mkanganyiko kwa wanafunzi. Hii inaweza kuwafanya wanafunzi kufikiria kwamba "mkulima hodari" ndicho kitenzi kishirikishi. Hata hivyo, kwa jinsi sentensi ilivyo, hatuwezi kupata muundo wa kitenzi kishirikishi peke yake. Mfano sahihi unaoakisi muundo uliotajwa ungekuwa kama *Mimi* ***siye***, *Yeye* ***ndiye*** n.k.

Pili, katika kufafanua kiarifu, utata unajitokeza pale prediketa inapochukuliwa kama kipashio cha kiarifu. Waandishi wa KKT 2021 wanasema kuwa "sehemu inayokaliwa na vitenzi katika sentensi huitwa prediketa (P)" kwa mifano ya (a) Mti mkubwa *umeangukia* nyumba (b) Chupa zote *zimetunzwa* kabatini (TET, 2021: 36). Fasili hii haitofautishii kati ya kitenzi na prediketa kama vipashio vya kiarifu. Hata hivyo, ushahidi unaonesha kuwa dhana ya prediketa ilitumiwa katika uchambuzi wa lugha wa mikabala ya mwanzo ya sarufi mapokeo na baadaye kadiri uchambuzi wa kimapokeo ulivyokuwa ukibadilika, dhana ya prediketa kurejelea kitenzi ilibadilika ambapo dhana ya "kiarifu" ilichukua nafasi

ikiwa sehemu ya sentensi inayoarifu juu ya kiima (Massamba na wenzake, 2012: 52-57; Ndumiwe, 2021: 66-68). Hivyo basi, prediketa (kiarifu) ni sehemu ya pili ya sentensi ambayo hutoa maelezo juu ya kiima katika mgao wa uwili wa sentensi (TUKI, 1990; Massamba, 2007). Hii inamaanisha kuwa dhana ya prediketa ni ya Kiingereza (predicate) na kwa Kiswahili ni kiarifu. Kuichukulia prediketa kama kipashio cha kiarifu kinachokaliwa na kitenzi/vitenzi ni kuchanganya wasomaji pia fasili hiyo inashindwa kuweka mpaka kati ya istilahi "kitenzi" na "prediketa". Inashauriwa kuwa badala ya kutumia istilahi "prediketa" kama mbadala wa kitenzi, itumike "kitenzi" na dhana ya prediketa isitumike kwa sababu ilishabadilika na kuibuliwa istilahi ya "kiarifu".

**3.2.5 Sentensi**

Katika kipengele hiki, utata unajitokeza kwenye fasili ya sentensi sahili na miundo yake, miundo ya sentensi ambatani na uchanganuzi wa sentensi.

**3.2.5.1 Sentensi Sahili na Miundo yake**

Sentensi sahili imefasiliwa kama sentensi yenye kitenzi kikuu kimoja au kirai kitenzi na hubeba wazo kuu moja (TET, 2021: 37). Fasili hii haitofautishi sentensi sahili dhidi ya aina zingine za sentensi kwa sababu kila sentensi huwa na kirai kitenzi. Pia, sentensi changamani inaweza kuwa na kitenzi kikuu kimoja na wazo kuu moja tu. Kulingana na mkanganyiko huu, ingefaa fasili ya sentensi sahili izingatie zaidi muundo wake ili kuitofautisha na zingine. Hivyo, ingefasiliwa kuwa, sentensi sahili ni sentensi ambayo huundwa na kishazi huru kimoja kinachotoa taarifa kamili (Matinde, 2012:158). Fasili hii inatofautisha kati ya sentensi sahili, changamani na ambatani kwa sababu sentensi changamani huundwa na kishazi tegemezi na kishazi huru ilhali sentensi ambatani hundwa na sentensi zaidi ya moja.

Kwa upande mwingine, katika kueleza miundo ya sentensi, ubainishaji wa vipashio vinavyojenga miundo ya sentensi sahili ni tata. Kwa mfano, katika KKT2021 imeelezwa kuwa sentensi sahili huweza kuundwa kwa namna anuwai kama Mfano Namba 8 unavyoonesha hapa chini.

8. (a) Kitenzi kikuu kimoja (T), mfano: Wanakijiji *walikata* mti.
   (b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (Ts+T), mfano: Karatasi *zilikuwa zimezagaa* kila
   mahali.
   (c) Vitenzi visaidizi viwili na kitenzi kikuu (Ts+Ts+T), mfano: *Tulidhani tutamkuta akicheza* mpira na Bakari hapa kwako.
   (d) Vitenzi visaidizi vitatu na kitenzi kikuu (Ts+Ts+Ts+T), mfano: Vijana *walikuwa wanataka kwenda kuomba* msaada wa chakula.
   (e) Kitenzi kishirikishi (t), mfano: Huu *si* mmea wa dawa ya watoto hata kidogo.

   **Chanzo**: TET (2021: 38).

Kulingana na Mfano Na. 8, maneno yaliyobainishwa kwa mlazo ni vipashio vya miundo ya sentensi sahili. Kwa kuchunguza data hiyo, mambo yafuatayo yanaibua utata. Kwanza, hakuna muundo hata mmoja unaohusisha kirai nomino dhahiri katika miundo hiyo kama katika sentensi ***Babu yangu*** *amepona*. Pili, inaonekana kuwa miundo ya sentensi sahili ni vitenzi tu si vipashio vingine vinavyoweza kuwa sehemu ya muundo wa sentensi sahili kama katika sentensi *Shughuli imeanza rasmi leo*. Tatu, katika sentensi hizo, msomaji anaweza kudhani kuwa maneno yaliyobainishwa kwa mlazo ndizo sentensi sahili jambo ambalo si kweli. Mwisho, sentensi zote hizo ni sahili ila miundo iliyotajwa haiakisi aina hiyo ya sentensi. Maelezo haya yanamaanisha kuwa kila muundo uliotajwa ulipaswa kujidhihirisha wenyewe bila kuambatana na vipashio vingine. Vinginevyo, muundo huo sio sahihi. Kufafanua hoja hii, tutumie miundo ya Mfano Na. 8(a)-(b). Katika mfano 8(a) sentensi ilipaswa kubainishwa kwa kitenzi peke yake kama *Walikata* na 8(b) ilipaswa kuwa *Zilikuwa zimezagaa* ili kuakisi uhalisi wa miundo yenyewe. Kwa hivyo, inashauriwa kuwa vipashio vinavyotajwa kujenga muundo wa sentensi ndivyo hivyo vinavyopaswa kuonekana na siyo vingine. Kuongeza vipashio vingine, kunabadili muundo uliobainishwa na kuwa mwingine.

**3.2.5.2 Miundo ya Sentensi Ambatani**

Kama tulivyoona katika sentensi sahili, ubainishaji wa mifano ya baadhi ya miundo ya sentensi ambatani unaleta utata. Nukuu ifuatayo inabainisha jinsi ambavyo miundo na mifano yake haioani.

9. (a) Sentensi changamani mbili na sentensi sahili mbili, mfano:
   (i) Alinunua mashuka yaliyofumwa na foronya zilizotariziwa.
   (ii) Ng’ombe aliyevunjika mguu amepona na mchungaji aliyekuwa anamhudumia ameondoka (TET, 2021: 40).

Mfano Na. 9 unadhihirisha sentensi zenye miundo ya sentensi changamani peke yake. Kila sentensi imeundwa na sentensi changamani na wala siyo sentensi changamani mbili na sahili mbili kama muundo uliotajwa. Mifano hii inamkanganya mwanafunzi hasa yule anayeamini na kukariri kila kilichoandikwa kwenye kitabu na ikizingatiwa kuwa ni kitabu cha kiada. Tunafikiri kuwa muundo uliotajwa hapo juu, mifano yake ingekuwa kama:

(i) Uliyemuona alikuwa hapa na alichobeba ni kikombe ila yule pale si yeye wala hukumuona.
(ii) Kelele unazosikia zinatokea huko na vigelegele vinavyosikika vinatokea huko pia lakini sauti ya ngoma haitoki huko hata mdundo huo sio wa huko.

Mifano (i)–(ii) iliyotolewa hapo juu inaakisi muundo wa sentensi changamani mbili na sahili mbili kama ulivyotajwa kwenye KKT2021.

### 3.2.5.3 Uchanganuzi wa Sentensi

Katika uchanganuzi wa sentensi kuna utata unaojitokeza pia. Kwanza, utata huo unahusu kuchanganya istilahi za mikabala tofauti, yaani, mkabala wa kimapokeo na wa kimuundo. Waandishi wanasema kuwa "uchambuzi wa kuzingatia mkabala wa kimapokeo (kidhima) huzingatia dhima ya kila kipashio katika tungo" (TET, 2021: 45). Maelezo haya yanamaanisha kwamba, kinachoongoza uchambuzi wa sentensi ni dhima za viambajengo vya sentensi husika. Akieleza maana ya viambajengo vya kidhima, Ndumiwe (2021:41) anasema ni vipashio vya kikazi vinavyounda sentensi ambavyo hurejelea kazi inayofanywa na kiambajengo husika katika tungo. Kwa kuzingatia mkabala wa kidhima, uchambuzi wa sentensi katika KKT2021 unabainishwa kupitia Mfano Na. 10.

10. Shehiza ni mwalimu

| S. Sahili | | |
|---|---|---|
| K | | A |
| | P | SH |
| N | t | N |
| Shehiza | ni | mwalimu |

**Chanzo**: TET (2021:42)

Katika Mfano Na.10, kuna utata wa kuainisha sentensi kimuundo ilhali mkabala unaotumika ni wa kidhima/kimapokeo ambao huzingatia dhima ya sentensi. Kulingana na Habwe na Karanja (2004:142), Matinde (2012:158) na Philipo (2018:176) sentensi huainishwa kimapokeo kwa kuzingatia dhima yake hususani ujumbe (maana) ambao sentensi husika huwasilisha na huweza kuainishwa kama sentensi taarifu, amri/agizi, ulizi, mshangao, shurutia n.k. Ikiwa sentensi inachanganuliwa kwa kuzingatia mkabala wa kidhima, hatua ya kwanza ilipaswa kuwa ni kutaja aina ya sentensi changanuliwa kwa kuzingatia dhima yake na si kuiainisha kimuundo. Uainishaji wa sentensi kama sahili, changamani na ambatani ni wa kimuundo unaozingatia sentensi imejengwa na vipashio gani. Kwa mantiki hii, tulitegemea sentensi "Shehiza ni mwalimu" itajwe kuwa ni "sentensi taarifu" au kama hiyo isingewezekana basi wachanganuzi wangeishia kusema ni "sentensi" kwa kuipa alama ya "S" kama ambavyo wachambuzi wa kileo wanavyofanya. Kwa mfano:

11. Sehiza ni mwalimu


| S | | |
|---|---|---|
| K | | A |
| N | t | SH |
| | | N |
| Shehiza | ni | mwalimu |

**Chanzo**: Uwandani (2023)

Uchanganuzi katika Mfano Na. 11 unaonesha kuwa sentensi imechanganuliwa kwa kutumia istilahi zinazotaja vipashio vya kidhima. Hii ni tofauti na ilivyooneshwa kwenye Mfano Na. 10 ambao ulichanganya istilahi ya kimuundo ya "sentensi sahili" na vipashio vingine vya kidhima vilivyoorodheshwa. Sambamba na hilo, utata mwingine unoajitokeza katika Mfano Na. 10 unahusu prediketa kuwa sehemu ya kiarifu (kiambajengo cha kiarifu) kikijengwa na kitenzi. Tatizo hili limekwishajadiliwa katika kipengele cha 3.2.4. Hoja hapa ni kwamba sentensi zichanganuliwe kimuundo ili kubainisha viambajengo vya kimuundo na kidhima ili kubainisha vipashio vya kidhima vya sentensi husika.

Pili, utata mwingine unaojitokeza uko katika uchanganuzi wa sentensi kwa mkabala wa kimuundo. Hapa, changamoto iko kwenye uchanganuzi wa kishazi tegemezi ambacho hupewa hadhi ya sentensi. Ili kuelewa hoja hii, tuone mfano mmowajapo.


12. Mtoto mzuri alifurahi alipopewa zawadi




**Chanzo**: TET (2021:49)

Kwa mujibu wa Mfano Na. 12, kishazi tegemezi kinapewa hadhi ya sentensi na kuchanganuliwa zaidi. Hii ni hali ya kawaida kwenye uchanganuzi wa kimuundo. Utata unaoibuka kutokana na mfano huo ni kitenzi kinachounda kishazi tegemezi kupewa hadhi ya kitenzi kikuu wakati kina kiambishi rejeshi kinachokifanya kutimiza majukumu ya kielezi. Kwa uchanganuzi huo, kitenzi *alipopewa* kina majukumu sawa na kitenzi kikuu *alifurahi*. Tunafikiri jambo hili si sawa kwa sababu ya kuwapo kwa kiambishi rejeshi katika kitenzi kinachojenga kishazi tegemezi. Ikiwa mchanganuzi alitaka kuichambua zaidi sentensi iliyoshushwa hadhi kwa kupachika kiambishi rejeshi, basi alipaswa kudondosha umbo la o-rejeshi na kitenzi kikawa *alipewa*. Kwa maana hiyo, uchanganuzi ungeonekana kama ifuatavyo:


13. Mtoto mzuri alifurahi alipopewa zawadi




**Chanzo**: Uwandani (2023)

Baadhi ya wanaisimu wa Kiswahili wamechanganua tungo changamani kwa namna iliyooneshwa katika Mfano Na. 13. Miongoni mwao ni Philipo (2018:185-186). Aidha, uchanganuzi wa namna hii unaondoa utata wa kukipa hadhi kitenzi rejeshi ya kuwa kitenzi kikuu. Namna nyingine ya kuchanganua sentensi changamani inayoweza kuondoa utata wa kukifanya kitenzi rejeshi kuwa kitenzi kikuu ni ule wa kutumia pembetatu zinazobeba kishazi chote. Kwa mfano:

14. Mtoto mzuri alifurahi alipopewa zawadi




**Chanzo**: Uwandani (2023)

Namna hii pia ya uchanganuzi wa sentensi inaondoa utata wa kitenzi rejeshi kupewa hadhi ya kitenzi kikuu na haijikiti katika kuchanganua zaidi kishazi tegemezi. Huu ndio uchanganuzi uliotumiwa na waandishi wengi wa sarufi ya Kiswahili kama Massamba na wenzake (2012:179-180) na Matinde (2012:178-180, 230).

**4.0 Hitimisho**

Makala hii imejadili utata unaojitokeza katika vitabu vya Kiswahili vya kiada vya kidato cha kwanza na tatu kwa shule za sekondari za Tanzania vilivyoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Makala imebaini kuwa kuna baadhi ya maelezo katika mada za sarufi ambayo yana mkanganyiko unaoleta utata kwa walimu na wanafunzi. Makala pia, imejaribu kuonesha maeneo yenye mkanganyiko na kutoa ushauri wa namna utata huo unavyoweza kuondolewa. Hata hivyo, makala inapendekeza kuwa kuna haja ya waandishi wa vitabu hivi kuvipitia upya na kwa umakini, kufanya uhariri wa kina na kubaini sehemu zenye utata na upungufu mwingine kisha kufanya marekebisho. Ikumbukwe kuwa wanafunzi wa ngazi ya sekondari ni wachache ambao wanaweza kubaini makosa au udhaifu uliomo vitabuni humo na kuuepuka bali wengi wao huchukulia kuwa kila kilichomo kitabuni ni sahihi.

**Marejeleo**

Bukagile, G. (2007). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari: Kidato cha Kwanza*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

GAO-PEMD. (1996). *Content Analysis: A Methodology for Structuring and Analyzing Written Materials*. Illinois: PEMD.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Haulle, E. na Kabelege, E. (2021). “Relevance and Quality of Textbooks Used in Primary Education in Tanzania: A Case of Social Studies Textbooks”. *Contemporary Education Dialogue.* 18 (1): 12-28.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Krippendorff, K. (2004). *Content Analysis: An Introduction to its Methodology*. Califonia: Sage Publications.

Ligembe, N.N. (2017). *Kitangulizi cha Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Afro Plus Industry.

Massamba, D.P.B. (2007). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Tol.2). Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Hokororo, J.I. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*, Toleo 4). Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia.* Mwanza: Serengeti Bookshop.

Ndumiwe, E.J. (2021). *Hadubini ya Sintaksia ya Kiswahili: Mwelekeo wa Nadharia na Vitendo*. Mwanza: Tridax Company Limited.

Nnamdi-Eruchalu, G.I. (2012). The Role of Textbooks in Effective Teaching and Learning of English as a Second Language. *Nigerian Journal of Curriculum and Instruction.* 20(1): 1-6.

Philipo, Z.T. (2018). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: CTP.

Radić-Bojanić, B.B. na Topalov, J.P. (2016). Textbooks in the EFL Classroom: Defining, Assessingand Analyzing. *Collection of Papers of the Faculty of Philosophy*. XLVI (3): 137-151.

TET (2010). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari: Kidato cha I-IV*. Dar es Salaam: TET.

____ (2021) *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Kwanza*. Dar es Salaam: TET.

____ (2021) *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tatu*. Dar es Salaam: TET.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

White, M.D. na Marsh, E.E. (2006). Content Analysis: A Flexible Methodology. *Library Trends* 55 (1), 22–45.